



## TANGAZO

### UUZAJI WA MAGOGO YA MTI AINA YA MKURUNGU KWA NJIA YA MNADA KATIKA KIJIKI CHA WACHAWASEME (IGAGALA No 9) NA KIJIKI CHA MPWAGA (IGAGALA No3) WILAYANI KALIUA MKOA WA TABORA

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) utauza magogo ya Mkurungu (*Pterocarpus tinctorius*) jumla ya vipande 7,456 vyenye jumla ya meta za ujazo 1,758.793. Magogo haya yapo katika Kijiji cha Wachawaseme na Mpwaga, Tarafa ya Igagala, wilaya ya Kaliua, Mkoani Tabora.
2. Magogo hayo ya Mkurungu yamepimwa na yamepangwa katika mafungu (Lots) 10 na yatauzwa kwa njia ya mnada wa hadhara kwa kuzingatia Kanuni ya 31 (ii) ya Kanuni za Sheria ya Misitu za Mwaka 2004. Magogo hayo yatauzwa mahali yalipohifadhiwa na jinsi yalivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.
3. Mnada utafanyika hadharani katika vijiji vya Wachawaseme na Mpwaga wakiwepo wanunuzi wote. Mnada utafanyika siku ya Jumatatu ya tarehe 20 Septemba, 2021 kuanzia saa 4:30 asubuhi.
4. Mnunuzi anakaribishwa kutembelea Kijiji cha Wachawaseme na Mpwaga kulipopangwa mafungu (loti) ya Magogo ya Mkurungu ili kukagua mazao hayo ya misitu muda wa kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri siku za Jumatatu hadi Ijumaa. Ukaguzi huo utafanyika kuanzia tarehe ya Tangazo hili hadi tarehe 19 Septemba, 2021. Aidha, Maafisa Misitu wa Wakala

(TFS) watakuwepo kwa ajili ya kutoa maelezo ya ziada ikiwa yatahitajika. Jedwali hili litatumika kuchagua fungu lenye magogo ya kununua kwa kuzingatia taarifa zilizo rodheshwa kama ifuatavyo:

**Jedwali na. 1: orodha ya mafungu (lots) za magogo katika vijiji vya Wachawaseme na Mpwaga**

Na	KIJILI	ENEO	Fungu (Lot Na)	IDADI YA MAGOGO	UJAZO (M3)	BEI(Tsh)/M <sup>3</sup>
1	Wachawaseme	A	1	752	171.745	700,000/=
			2	752	175.034	
			3	586	138.027	
			4	509	110.543	
			5	871	206.414	
		B	6	543	114.972	
			7	1041	230.656	
			8	1258	337.108	
		C	9	607	151.844	
2	Mpwaga	D	10	537	122.444	
<b>JUMLA KUU</b>				<b>7,456</b>	<b>1758.793</b>	

5. Wakala wa Huduma za Misitua Tanzania utatoa barua ya ushindi kwa mnunuzi aliyeshinda mnada wa kila fungu.

6. Mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25 %) ya thamani yote ya ununuzi siku ya mnada. Fedha hizo hazitarudishwa endapo mshindi atashindwa kulipia ujazo wote aliouziwa. Aidha, asilimia sabini na tano (75 %) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia siku ya tarehe ya toleo la barua ya ushindi kwa mnunuzi. Malipo yote yafanyike kupitia benki au mitandao ya watoa huduma za kifedha baada ya kupewa hati ya madai (bill) kutoka Mfumo wa Makusanyo ya Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT Portal) itakayotolewa na Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitua Tanzania (TFS)-Kaliua.

7. Atakayeshinda fungu husika atalazimika kulipia ushuru wa asilimia tano (5%) ya mazao hayo kwa Halmashauri ya wilaya Kaliua.

8. Mnunuzi aliyeshinda mnada atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100. Baada ya tarehe hizo ulinzi wa mazao hayo yatakuwa juu ya mnunuzi mwenyewe.

9. Mnunuzi aliyeshinda atapaswa kuwasilisha hati ya malipo (pay-in-slip) kwa Mhifadhi Misitu Wilaya ya Kaliua kama uthibitisho wa malipo na siyo zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

10. Usajili wa wanunuzi na watazamaji wenye nia ya kushiriki mnada utafanyika katika Kijiji cha Wachawaseme na Mpwaga kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa nne kamili (4:00) asubuhi siku ya mnada. Aidha, wanunuzi watakochelewa kuwasilisha nia zao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika mnada.

11. Aidha, kibali cha kusafirisha magogo nje ya nchi kitatolewa kwa tangazo maalum la serikali (Government Notice) kwa mshindi atakayehitaji kusafirisha magogo hayo nje ya nchi.

12. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti zifuatazo za: [www.tfs.go.tz](http://www.tfs.go.tz) na [www.mnrt.go.tz](http://www.mnrt.go.tz).

**Limetolewa leo 05 SEPTEMBER 2021**  
**na**  
**KAMISHNA WA UHIFADHI**  
**WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA**  
**S. L. P 40832**  
**DAR ES SALAAM**